

# uzalishaji wa viungo na pato la mkulima

## mafunzo kutoka Amani, Tanga

TARP II – SUA Project

# Uzalishaji wa Viungo na Pato la Mkulima

## Mafunzo kutoka Amani, Tanga

---

Ziara hii ilitayarishwa na
**Kamati ya Utekelezaji wa Mradi wa**

**Uhakika wa Chakula na Pato la Kaya kwa Wakulima Wadogowadogo Tanzania: Mradi wa Utafiti Unaotilia Mkazo Wanawake**

Mradi huu upo chini ya Mradi wa Taifa wa Utafiti wa Kilimo, Awamu ya Pili
(TARP II – SUA Project)

**June 2002**

**Waandishi**

Dk. J. G. Lyimo-Macha
Prof. R.E. Malimbwi

**Wahariri**

Kamati ya Mradi:

Prof. L. D. B. Kinabo
Prof. A. J. P. Tarimo
Prof. E. Batamuzi
Dk. P. J. Makungu

**ISBN: 9987 605 46 X**

**Kimechapishwa na:**

Mradi wa Uhakika wa Chakula na Pato la Kaya kwa
Wakulima Wadogowadogo, Tanzania (TARP II – SUA Project)
Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo
SLP 3151
Chuo Kikuu, Morogoro
Simu: +255 23 2600970 au +255 23 2603511 ext. 4251

Toleo Namba: TS2 - 48

**© 2002 TARP II – SUA Project**

Mbunifu wa Jalada - L.D.B. Kinabo: Picha inawaonesha wakulima wakipata elimu kutoka kwa wenzao juu ya uzalishaji wa viungo kama njia mojawapo muhimu ya kuongeza kipato cha kaya

# Yaliyomo


| | | |
|---|---|---|
| | *Dibaji* | *v* |
| | *Vifupisho* | *vii* |
| **1.0** | **Utangulizi** | **1** |
| **2.0** | **Mashamba ya viungo** | **2** |
| | 2.1 Bustani ya Kakao Kizugu | 2 |
| | 2.2 Bustani ya miche | 4 |
| | 2.3 Mashamba ya wakulima | 4 |
| | 2.4 Shamba la chai | 5 |
| **3.0** | **Mambo muhimu kutokana na ziara** | **6** |
| | 3.1 Waliyojifunza | 6 |
| | 3.2 Waliyoahidi kutekeleza | 7 |
| **4.0** | **Maoni** | **8** |
| | 4.1 Washiriki | 8 |
| | 4.2 Wakulima wa Amani | 8 |
| | 4.3 Wawezeshaji | 8 |
| **5.0** | **Viambatisho** | **10** |
| | 5.1 Washiriki | 10 |
| | 5.2 Orodha ya viungo | 11 |
| | 5.3 Ratiba ya ziara | 13 |

# Dibaji

Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo na Uhakika wa Chakula (MAFS), pamoja na Chuo Kikuu cha kilimo cha Norway (NLH), kinatekeleza Mradi wa Uhakika wa Chakula na Pato la Kaya kwa Wakulima Wadogo wadogo Tanzania.

Lengo mojawapo katika mradi huu ni kuimarisha uhusiano kati ya Wakulima, Watafiti na Washauri wa Ugani. Ili kufikia lengo hili, mradi umepanga utaratibu wa kuwawezesha wakulima kutembeleana ndani ya kanda zao na kati ya kanda na kanda.

Makala hii inawasilisha ripoti ya ziara moja iliyofanyika mwishoni mwa mwezi Aprili 2002. Ziara hii iliwashirikisha wakulima na washauri wa ugani kutoka wilaya ya Morogoro Vijijini, waliowatembelea wakulima wa viungo mbali mbali wa Amani, wilaya ya Muheza, Tanga. Taarifa hii pia inapatikana katika lugha ya Kiingereza.

Profesa L. D. B. Kinabo
Mratibu Mradi, TARP II-SUA
June 2002

# Vifupisho

| | |
|---|---|
| ARI | Taasisi ya Utafiti wa Kilimo |
| MAFS | Wizara ya Kilimo na Uhakika wa Chakula |
| NLH | Chuo Kikuu cha Kilimo cha Norway |
| NORAD | Shirika la Maendeleo la Norway |
| SUA | Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo |
| TARP II | Mradi wa Taifa wa Utafiti wa Kilimo Awamu ya Pili |

# 1.0 UTANGULIZI

Mradi wa Uhakika wa Chakula na Pato la Kaya ukitilia mkazo zaidi shughuli za kina mama umeweka mikakati mbalimbali ya kuweza kufanikisha azma ya kuinua kipato cha mkulima mdogomdogo Tanzania. Mojawapo ya mikakati hiyo ni kuelimisha wakulima kwa njia mbali mbali kama vile mafunzo ya darasani/ukumbini, shambani au kwenye maabara yaliyopo kwenye vituo vya utafiti. Mafunzo ya shambani yamegawanyika katika sehemu mbili, shambani na ziara kwa wakulima wenzao.

Ziara za mafunzo kwa wakulima chini ya mradi huo zimekuwa zikiendelea kama zilivyopangwa. Wakulima, wafugaji, wataalamu wa ugani na watafiti katika kanda za Nyanda za Juu Kusini na Mashariki wamekuwa wakipata nafasi za kutembelea wenzao katika kanda hizo ili kujifunza mambo mbali mbali. Mwezi wa tatu, mwaka 2002 ilifanyika ziara ya wakulima kutoka Morogoro, kanda ya mashariki kutembelea wenzao wa kanda ya hiyo huko wilayani Muheza, Tanga (kiambatisho 1). Lengo kuu lilikuwa kuwapatia nafasi wakulima wa pande zote kujifunza kwa vitendo na nadharia kuhusu shughuli za uzalishaji wa viungo mbali mbali.

Wakulima walioteuliwa kutoka Morogoro wanajulikana kuwa ni wazalishaji wa viungo kama vile iliki, karafuu, pilipili manga, mdalasini n.k. Hawa walipatiwa nafasi kuwatembelea wakulima wa Amani Tanga ambao ni maarufu kwa uzalishaji na uuzaji wa viungo hivyo na vinginevyo.

Ziara ilifanyika wilayani Muheza, maeneo yaliyotembelewa ni katika mashamba ya viungo mbali

mbali. kitengo cha uzalishaji wa miche ya viungo na shamba la chai.

Wakulima 12 (wanawake 6 na wanaume 6) na wataalamu wa ugani 2 kutoka tarafa za Mkuyuni na Matombo, wilayani Morogoro Vijijini walishiriki katika ziara hiyo (Kiambatisho 3). Kwa ujumla ziara ilikuwa ya mafanikio kwani wakulima walijifunza mengi kuhusu kilimo cha viungo. matumizi ya ziada na mbinu za utafutaji soko la viungo.

Katika makala hii maelezo yametolewa kuhusu uzalishaji wa viungo mbali mbali, utafutaji wa soko na mapendekezo ambayo wakulima wameahidi kuafanyia kazi kutokana na ziara hii.

## 2.0. MASHAMBA YA VIUNGO

### 2.1. Bustani ya Kakao Kizugu

Shamba la Kizugu lililoko Amani hujishughulisha na kilimo cha kakao chini ya kitengo cha uzalishaji miche ya viungo cha ARI Mlngano. Kakao inayolimwa hapo ililetwa toka Nigeria, Trindad na Ghana tangu 1959. Kakao ni zao ambalo bado ni geni katika sehemu nyingi za Tanzania na ndio linaanza kuendelezwa zaidi kipindi hiki. Zao hili hutumika kama kinywaji, kwenye vipodozi, pipi, chokoleti na kutengenezea madawa. Zipo aina (varieties) kuu tano za kakao zinazolimwa na kuzalishwa katika shamba hili, nazo ni T60, ICS95, DR1, DR2 na DR38.

Miti ya mikakao hukua vizuri katika maeneo yenye udongo tifutifu, wenye mbolea (samadi au vunde) na kivuli cha kutosha. Tunda la kakao lililoiva (ambalo halijakauka) hupandwa kwa kulaza, sentimita 2.5 toka tunda moja hadi lingine katika vitalu vyenye vumbi la mbao au pumba za mpunga. Kisha hufunikwa na kumwagiwa maji. Baada ya

siku 12-21 zinakuwa zimechipua kama mche wa harage (kabla ya kutoa jani) ndipo huhamishwa na kuoteshwa kwenye viriba vya migomba, au plastiki vyenye udongo na mbolea na kupangwa kivulini. Miche hukaa katika viriba kwa kipindi cha miezi 9 hadi mwaka mmoja kabla ya kuhamishiwa katika mashamba.

Sharti kuu la ulimaji wa zao hili ni kuandaaa shamba mapema, liwe na rutuba ya kutosha pamoja na miti ya kivuli. Miti ambayo inaweza kuotesha na kakao ni kama vile migomba, miwese au mibaridi/misaji. Vipimo vya umbali wa kuotesha mche hadi mche pia ni jambo la kuzingatia ili miti ikue, itoe mazao mazuri na kuzuia moto na wadudu. Nafasi inayopendekezwa ni meta 4 x 4 kwa mbegu kubwa kama T60, ICS95 na meta 2 x 4 kwa mbegi ndogo kama DR 1, DR 2 na DR 38. Shimo la kupanda mche wa kakao liwe na kina cha sentimeta 60 (ft2) urefu na upana wa sentimeta hizo hizo. Utunzaji kwa njia ya palizi ni muhimu. Shamba likitunzwa vyema mazao huwa tayari baada ya miaka mitatu hadi mitano.

Soko la kakao ni huria, wakulima wanaojishughulisha na kilimo cha kakao wamekiri kuwa soko sio tatizo kwao. Bei ya chini kabisa ni shilingi mia nne (Tshs 400/=) kwa kilo na mti mmoja hutoa kilo 20-30 kwa mwaka. Kwa kuzingatia umbali wa kupanda wa meta 4 x 4 ina maana kutapatikana miche 625 kwa hekta moja na hivyo mkulima anaweza kupata shilingi milioni tano (Tshs 5.000.000/=) kwa mwaka.

## 2.2. Bustani ya miche ya viungo

Bustani ya miche ya viungo iliyopo Amani inajulikana kwa jina la "Spice trail". Kwa miaka mingi imekuwa ikimilikiwa na kusimamiwa na taasisi ya utafiti wa kilimo, Mlingano. Hivi sasa bustani hiyo imekabidhiwa Taasisi ya Utafiti wa Wadudu Waharibifu (TPRI) Arusha, ingawa wafanyakazi waliokuwepo tangu awali bado ndio wahusika wakuu wa kitengo hicho.

Bustani hii ina miche mbali mbali ya viungo vifuatavyo; iliki, mdalasini, pilipili manga, pilipili mtama, binzari, karafuu, tunda tamu (*garcinia mangostana*), tunda chachu, tangawizi, michikichi/miwese, langilangi (*cananga odorata*), vanilla, vipera chachu (strawberry guava/ *psdium oathiemum*), mang'ong'o (*spondias cythclas*), mifenesi, carambola, shelisheli, kiungo kamili (allspice) na mbilimbi (*averhoa bilimbi*) nk. (Kiambatisho 2). Miche inapokuwa tayari huuziwa watu binafsi na pia mashirika mbali mbali.

Kitengo hicho cha ustawishaji wa miche ya viungo pia kina eneo la shamba la miti ya viungo hivyo iliyooteshwa na kustawishwa kutumia kilimo cha kutotifua udongo na kutopalilia (No/zero tillage system). Miti iliyostahili kupandwa sehemu zenye kivuli ilichanganywa na miti asili na pia miti ya matunda ambayo inatumika kama kivuli na kama sehemu ya kuegemewa na mimea ya viungo kama vile pilipili manga na vanilla ambayo huhitaji miti ili ijiegemeze/ijishike/ijitundike.

## 2.3. Mashamba ya wakulima

Wakulima wengi wa iliki, pilipili manga, karafuu na viungo vingine wamepanda miti ya viungo bila kutifua

udongo na baadhi wametumia kilimo mseto. Wakulima wanafahamu kwamba kilimo mseto huhifadhi ardhi. Aidha mazao ya aina nyingi hupatikana katika eneo moja jambo ambalo ni muhimusehemu zenye uhaba wa ardhi kama Amani.

Wakulima wa Amani wanaelewa kuhusu upandaji hadi uvunaji wa mimea ya viungo, na hii ni kwa kila kiungo na pia kuhusu hifadhi na uuzaji (soko). Aidha wakulima hutumia aina mbalimbali za mbolea katika mashamba yao ambazo ni pamoja na samadi ya ng'ombe, mbuzi na melele (vinyama pori). Pamoja na uzoefu walionao, wakulima pia hufaidika kutoka kwa wataalamu wa ugani na wafanyakazi wa kitengo cha bustani ya miche.

Zao kuu la biashara kwa wakulima waliowengi ni iliki ambayo huuzwa hadi shilingi elfu tano (Shs 5,000/=) kwa kilo moja. Walikuwa na chama chao cha ushirika ambacho kiliwasaidia sana katika kutafuta na kuwapatia soko la iliki. Kwa sasa chama hicho hakipo tena na wakulima wanajitafutia soko lao wenyewe. Walibaini umuhimu wa kuwa na vikundi vya wakulima ili kuboresha uzalishaji na biashara ya viungo.

## 2.4. Shamba la chai

Shamba la chai la Amani hushughulika na uzalishaji wa chai kuanzia kwenye vitalu bustanini, shambani hadi ukaushaji kiwandani, usindikaji na hatimaye kufunga majani ya chai tayari kwa mauzo. Wakulima walijionea hatua kwa hatua tangu utayarishaji wa viriba vya kuoteshea chai hadi hatua ya kufunga katika mifuko (viroba) tayari kwa kusafirisha kupelekwa bandari za Mombasa au Dar es Salaam tayari kwa kusafirishwa ng'ambo.. Pia walipewa maelezo kuwa soko la chai sio tatizo kwani yapo mashirika

ya ndani na nje ya nchi yaliyotayari kununua chai mradi ubora wa chai uwe umetiliwa mkazo.

Chai ni zao geni kwa wakulima wengi walioshiriki katika ziara hii ingawa baadhi yao (wakulima toka Tawa) wanayo miti ya michai kijijini kwao iliyokuwa imepandwa na Wajerumani miaka mingi iliyopita, ila hawakujua kuwa ndio inayotoa majani ya chai.

Mashamba ya chai ya Amani huhudumiwa na wakulima waishio jirani wakifanya kazi kama vibarua. Pia wakulima hao huajiriwa kwa msimu katika kiwanda hicho. Shughuli hizi ni muhimu sana kwa wakulima hao kwani licha ya wao kuuza chai yao kiwandani hapo wanaongeza pato lao kwa kufanya kazi kwenye mashamba hayo na pia kiwandani.

## 3.0. MAMBO MUHIMU KUTOKANA NA ZIARA

### 3.1. Waliyojifunza

- Utayarishaji wa vitalu na shamba la kakao
- Upandikizaji wa kakao na miti ya kivuli inayofaa katika shamba la kakao
- Utayarishaji wa viriba kwa ajili ya miche ya viungo na chai
- Utengenezaji wa viriba kutumia mianzi, majani makavu ya migomba na makuti
- Jinsi ya kuchuma chai
- Utunzaji wa ardhi/udongo kwa kutumia kilimo cha kutotifua na kutopalilia shamba
- Kilimo mseto; kuchanganya miti ya viungo na miti ya matunda kwa ajili ya kivuli na kuhifadhi ardhi

- Jinsi ya kupanda mbegu za kakao katika vumbi la mbao
- Utunzaji wa iliki zenye mikole mirefu na uchumaji wake
- Upandaji bora wa miti ya viungo kufuata vipimo na nafasi inayotakiwa
- Jinsi ya kutumia samadi ya mbuzi na wanyama pori (nguchiro na pelele) ili kurutubisha ardhi
- Uvunaji bora wa mdalasini (kubambua magome)
- Umuhimu wa kuotesha miti ili kuhifadhi mazingira ikiwa ni pamoja na vyanzo vya maji
- Upandaji bora wa pilipili manga na matumizi ya miti mifupi ili kurahisisha uvunaji wake
- Umuhimu wa kuwa na vikundi vya wakulima ili kupata soko na pembejeo kwa urahisi.

### 3.2. Waliyoahidi kutekeleza baada ya ziara

- Kuanzisha miradi ya kuotesha miche ya mikarafuu na mdalasini
- Kupanua shamba lake ili kuongeza miti ya viungo
- Kuhamasisha uundaji wa vikundi vya wakulima wa viungo
- Kuboresha kilimo cha viungo kwa kutumia mbolea ya wanyama pori na mboji
- Kuanzisha kitalu cha mikarafuu
- Kuhamasisha wengine kuendeleza kilimo cha viungo na kutafuta soko la pamoja
- Kuhifadhi mazingira
- Kuanzisha kikundi cha wakulima wa chai ili kufanya jaribio la kuanzisha shamba la chai
- Kuendeleza shamba la mikarafuu
- Kutunza vema shamba la viungo

- Kutengeneza bustani ya miche na kutengeneza viriba
- Kupanda miti kwenye shamba la iliki kwa ajili ya kivuli

## 4.0. MAONI

4.1. Washiriki wa ziara wamekiri kuwa wamejifunza mengi mapya ingawa wao pia ni wakulima wa viungo, wamepata ujuzi mpya hasa katika:

- Utayarishaji wa shamba, mbegu, miche na upandaji wa miche shambani kwa kufuata vipimo
- Uchaguzi wa mbegu bora kuliko wanazozitumia
- Utunzaji wa mashamba ya viungo na matumizi ya mbolea (samadi na mboji)

4.2. Wakulima wa Amani kwa upande wao nao wamejifunza umuhimu wa kuunda vikundi ili kutafuta soko la mazao yao kwa pamoja.

4.3. Wawezezashaji wa ziara wameona kuwa ziara hii ilikuwa muhimu kwa wakulima wa viungo kutoka Morogoro kwa kuwa waliweza kupata mafunzo mengi, ikiwa ni pamoja na kujua mbegu bora, za muda mfupi na zenye kuweza kupata soko kwa urahisi. Pia wamepatiwa majina ya wanunuzi ambao kama wakiweza kujiunga pamoja wanaweza kupata mnunuzi mzuri wa mazao yao. Wawezeshaji wamewaahidi wakulima kuwa watapanga muda wa kwenda kufauatilia maazimio yaliyowekwa na wakulima.

Wawezeshaji pia walipata fursa ya kushauriana na uongozi wa kiwanda/shamba la chai Amani kuhusu uwezekano wa kufanya utafiti huko Nyachiro na Tawa ili kuona kama kuna uwezekano wa kuendeleza kilimo cha chai ambacho kilikuwa kianze zamani. Pia kuona kama kuna uwezekano wa kuanzisha kiwanda kidogo cha kukausha chai itakayopatikana huko. Ingawa jambo hilo ni la muda mrefu kidogo laweza kuwa mkakati mzuri wa kuwaongezea pato wakulima wa sehemu hizo.

## 5.0 VIAMBATISHO

### 5.1 Washiriki

| Na. | Jina | Kazi | Kijiji | Kata | Anuani |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Geroda Amani | Mkulima | Konde | Kisemu | S.L.P. 640 Morogoro |
| 2 | Yahya Kondo | Mkulima | Kibogwa | Kibogwa | S.L.P. 1880 Morogoro |
| 3 | Peter Chamagomba | Mkulima | Tawa | Tawa | S.L.P. 1880 Morogoro |
| 4 | Safia Hamadi | Mkulima | Kibogwa | Kibogwa | S.L.P. 1880 Morogoro |
| 5 | Ramadhani Changango | Mkulima | Nyachiro | Kibogwa | S.L.P. 1880 Morogoro |
| 6 | Christina John | Mkulima | Tawa | Tawa | S.L.P. 1880 Morogoro |
| 7 | Ayubu Salum | Mkulima | Kinole | Matombo | S.L.P. 1880 Morogoro |
| 8 | Monica Emil | Mkulima | Nyachiro | Kibogwa | S.L.P. 1880 Morogoro |
| 9 | Vitalis Mbena | Mkulima | Konde | Kisemu | S.L.P. 1880 Morogoro |
| 10 | Hassan Dikinga | Mkulima | Nyachiro | Kibogwa | S.L.P. 1880 Morogoro |
| 11 | Aziza Athumani | Mkulima | Kibogwa | Kibogwa | S.L.P. 1880 Morogoro |
| 12 | Fatuma Ramadhani | Mkulima | Kinole | Matombo | S.L.P. 188 0 Morogoro |
| 13 | Andrew Mandia | MUK | . | Tawa | S.L.P. 747 Morogoro |
| 14 | Herriel Amir | MUK | | Kisemu | S.L.P. 747 Morogoro |

* MUK –Mtaalamu wa Ugani wa Kata/Kijiji

## 5.2. Orodha ya viungo

### Orodha ya Misingi ya Uhusiano ya Viungo Muhimu Vilivyopo Katika Bustani ya Zigi, 25 Julai, 1996

| Jina la kisayansi | Jina la kawaida | Jina la Kiswahili | No. |
|---|---|---|---|
| **A: Viungo:** | | | |
| 1. Cinnamon zeylanicum | Cinnamon | Mdalasini | 50 |
| 2. Elletaria cardamonum | Cardamon | Iliki | 0.5ha |
| 3. Eugenia aromatica | Cloves | Karafuu | 40 |
| 4. Myristica fragrans | Nutmeg | Kungumanga | 4 |
| 5. Piper nigram | Black pepper | Pilipili manga | 100 |
| 6. Vinnila latifolia | Vanilla | Vanilla | 9 |
| **B: Matunda na Kokwa:** | | | |
| 1. Annona muricata | Sour sop | Stafeli | 3 |
| 2. Annona reticulata | Bullocks heart | Topetope | 2 |
| 3. Artocarpus integrifolia | Jack fruit | Fenesi | 1 |
| 4. Artocarpus odoratisima | - | Shelisheli | 1 |
| 5. Artocarpus utilis | Bread fruit | Shelisheli | 6 |
| 6. Artocarpus heterophylus | Bread fruit | Shelisheli | 1 |
| 7. Averhoa bilimbi | Bilimbi | Mbilimbi | 2 |
| 8. Averhoa carambolla | Carambola | Karambola | 4 |
| 9. Areca catecho | Batelnut | Popoo | 7 |
| 10. Cola nitilda | Cola nut | Cola | 6 |
| 11. Chrysobalanas cainito | Star apple | - | 2 |
| 12. Chrysobalanas icaco | US coco plum | - | 3 |
| 13. Dillenia indica | Elephant fruit | - | 4 |
| 14. Eugenia malacensis | Malay apple | - | 6 |
| 15. Eugenia domestica | - | - | 6 |
| 16. Eugenia uniflora | Pitang cherry | - | 3 |
| 17. Garcinia mango stana | Mangostein | Tuna tamu | 10 |
| 18. Lucuina salisfolia | Canistel | Zeituni | 6 |
| 19. Mammea americana | Mammey apple | - | 3 |
| 20. Macadamia ternifolia | Macadamia nut | - | 1 |
| 21. Nephelium litchi | Litchee | Hichi | 3 |
| 22. Passiflora quadrangulis | Sour granadilla | Papai kamba | 1 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 23. Passiflora edulis | Passion fruit | Makakara | 1 |
| 24. Psidium cattleianum | Straw berry | Mapera | 10 |
| 25. Psidium guajava | guava | Mapera | 10 |
| 26. Punica granatum | Common guava | Komamanga | 2 |
| 27. Persia americana | Pommegranate | Parachichi | 10 |
| 28. Spondius lutes | Avocado | Sambia | 2 |
| 29. Spondius cytherea | Mombin plum | Ngongo | 8 |
| 30. Terminalia catapa | Mombin plum | Mkungu | 4 |
| 31. Mangifera indica | Indian almond | Mwembe | 4 |
| 32. Macadamia ternifolia | Mango | - | 1 |
| 33. Prunus domestica | Macadamia nut | - | 7 |
| **A: Mbegu za mafuta.** | Peaches | Nil | |
| 1. Arenga pinnata | Sugar palm | Nil | |
| 2. Acacia fernanciana | Cassia oil | Mlanga langa | |
| 3. Cananga odorata | Ylang ylang | Nil | 10 |
| 4. Pimmenta acris | All spice | Nil | 3 |
| 5. Cymbopogon citrates | Lemon grass | Nil | 10 |
| 6. Pentadesma butyraceae | - | Mawese | 6 |
| 7. Elaies guinensis | African palm oil | Machachu | 1 |
| 8. Garcinia Xantomonas | - | Nil | 6 |
| 9. Ressia edulis | - | Nil | 10 |
| 10. Jambos jambosa | Rose apple | Nil | 2 |
| 11. Pasgvelia latifolia | - | Nil | 4 |
| 12. Canarium communea | Java almond | | 4 |
| | | | 1 |
| **B:Mingine:** | | | 1 |
| 1. Bixa olerana | | Nil | 6 |
| 2. Diospyros mollis | Dye | Black silk dye | |
| 3. Cresentia cujete | Ebenester Dye | | |
| 4 Carcimilowa edulis | - | | 6 |
| | - | | 1 |
| **C: Aina zilizopotea (Viungo)** | | | 2 |
| 1. Curcuma longa | | Binzari | 3 |
| 2. Zingibar officinalis | Turmeric | Tangawizi | |
| 3. Cinnamon camphora | Ginger | Karafuu maiti | |
| | - | | |
| **D: Matunda na Kokwa:** | | Nil | |
| 1. Achras sapota | Sapoddila | Nil | |
| 2. Eriabotrya japonica | Loquat | Nil | |
| 3. Feijoa sellowiana | Feijoa | Nil | |
| 4. Pasiflora ligularis | Sweet granaddila | Mapera meupe | |
| 5. Psidium gvajava | White guava | Kakara | |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 6. | Black passion fruit | Passion fruit | Nil |
| 7. | Annona squamosa | Squamesa | Nil |
| 8. | Annona cherimoya | Cherimoya | Zabibu |
| 9. | Vitis spp | Grape fruit | Chai |
| 10. | Catha edulis | Arabian tea | Nil |
| 11. | Prunus persica | Pears<br>Apples | Nil |

## 5.3. Ratiba ya ziara 24/4/2002-28/4/2002

| Tarehe | Shughuli | Mahali | Wahusika |
|---|---|---|---|
| 24/4/2002 | - Washiriki kuwasili Muheza | - Muheza | - Washiriki wote na wawezeshaji |
| 25/4/2002 | - Kutembelea shamba la Kizugu | - Kizugu (Amani) | - Washiriki, wawezeshaji na Bw. Mandoshe |
| | - Kutembelea bustani ya miche | - Zigi | - Washiriki. wawezeshaji na Bw. Selemani |
| 26/4/2002 | - Kutembelea mashamba ya wakulima | - Zigi Juu | - Washiriki. wawezeshaji na Bw. John Lyimo |
| | | - Kisiwani (Mavumbi) | - Washiriki. wawezeshaji. Familia ya Sangai na Bw. J. Kiluwa |
| 27/4/2002 | - Kutembelea shamba na kiwanda cha chai | - Amani | - Washiriki. wawezeshaji na Bw. K. Kabage |
| 28/4/2002 | - Majumuisho | - Tanga | - Washiriki na wawezeshaji |
| | - Kusafiri kurudi Morogoro | | Wote |